



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

CHUO CHA UHASIBU ARUSHA



TANGAZO LA KOZI FUPI YA

KUBORESHA UTENDAJI KAZI NA MAWASILIANO KWA WAHUDUMU WA OFISI NGAZI YA I NA II

(08 – 12 Aprili 2019 – IAA, Arusha)

1.0 UTANGULIZI

Kozi hii imeandaliwa mahususi kwa ajili ya kuleta maboresho, tija na ufanisi wa kazi kwa Wahudumu, Walinzi na Wafanya Usafi katika Taasisi wanazotumikia. Wahudumu, Walinzi na Wafanya Usafi wamekuwa kiungo muhimu katika taasisi nyingi kwa uwajibikaji wao na kuweza kufikia malengo ya taasisi. Ikiwa mafunzo mafupi ni sehemu ya kuboresha kazi zao, ni mategemeo yetu kwamba baada ya kozi hii watakuwa na elimu ya ziada katika utendaji na uwajibikaji wa kazi zao za kila siku.

2.0 MALENGO YA KOZI

Mwisho wa kozi hii mshiriki atakuwa na uelewa mpana katika maeneo yafuatayo:

HATUA YA KWANZA

- (a) Muundo wa Taasisi anayofanyia kazi;
- (b) Wajibu wa Mhudumu, Mlinzi na Wafanya Usafi;
- (c) Kupokea, kutoa na kutekeleza maagizo;
- (d) Maadili ya kazi;
- (e) Ubebaji wa nyaraka na majalada ya ofisi;
- (f) Ushirikiano na uwajibikaji;
- (g) Jinsi ya kuweka malengo ya kazi na kuyafikia;
- (h) Matumizi mazuri ya muda eneo la kazi
- (i) Kukabiliana na changamoto za kazi na Teknolojia;
- (j) Huduma za masijala kwa mtandao (E- records);
- (k) Uandishi wa ripoti; na
- (l) Mahusiano bora katika ofisi.

HATUA YA PILI

- i) Utunzaji wa siri za ofisi
- ii) Kuwasiliana kwa njia ya mtandao (e-mail for office communication)
- iii) Umuhimu wa 'dispatch'
- iv) Kumbukumbu za nyaraka (Records of documents/files)

3.0 NANI ANAPASWA KUHUDHURIA

Kozi hii ni maalumu kwa Wahudumu, Walinzi na Wafanya Usafi wa ofisi na watoa huduma wote waliopo katika Taasisi.

4.0 MBINU YA UFUNDISHAJI

Kozi hii itafundishwa kwa njia mbalimbali ikiwemo ya utoaji mihadhara, majadiliano, uchunguzi kifani na njia ya vitendo ili kuboresha tija katika Taasisi.

5.0 ADA YA KOZI NA NAMNA YA ULIPAJI

Ada ya kozi ni kiasi cha **Shs 900,000/= (Laki Tisa tu)**. Ada hii ni kwa ajili ya vitini vya mafunzo, chai, chakula cha mchana na gharama za safari ya kwenda mbuga za wanyama. Malipo hayo yafanyike moja kwa moja kwenda Chuo cha Uhasibu Arusha (Institute of Accountancy Arusha), kwenye Akaunti Namba **014103007130 NBC, Tawi la Arusha** kwa njia ya fedha taslimu, hundi au TISS.

6.0 TAREHE NA MAHALI PA MAFUNZO:

Kozi hii itaendeshwa kuanzia tarehe 08 – 12 Aprili 2019, Chuo cha Uhasibu Arusha, Kampasi kuu iliyopo Njiro Arusha.

7.0 MAWASILIANO

Kwa mawasiliano na maelezo zaidi wasiliana na:

Mkurugezi Wa Kozi

Ms. Lilian Minja Barua pepe iminja@iaa.ac.tz & Lilysta19@yahoo.com
Simu Na.: 0713214513 and 0767214513

Kaimu Mkuu wa Idara – Ushauri wa Kitaalamu na Kozi za Kujiendeleza

Pamela Chogo Barua Pepe: pchogo@iaa.ac.tz & pamsekela@gmail.com
Simu Na: +255 655 611512 & +255759334659

Msimamizi wa Kozi

Caroline Lucumay Barua Pepe: clucumay@iaa.ac.tz & lucumayc@gmail.com
Simu Na: +255 782 993 077 & +255 652 379 888

MAOMBI YAKO YATUMWE KWA:

Mkuu wa Chuo
Chuo cha Uhasibu Arusha
S. L. P. 2798
ARUSHA
Barua Pepe: iaa@iaa.ac.tz